**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

P. O. BOX232 TUKUYU.

SHULE YA SEKONDARI KAYUKI,
S.L.P 232,
**TUKUYU**.
09/04/2022

FOMU YA KUJIUNGA INAPATIKANA
SHULENI
NAMBA ZA SIMU,
MKUU WA SHULE **0754074440,**
MAKAMU MKUU WA SHULE **0765797584,**
MATRON **0764076662,**
MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI,

…………………………………………,

………………………………………….,

S.L.P ……………………………………,

…………………………………………..,

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KAYUKI HALMASHAURI YA RUNGWE MKOA WA MBEYA MWAKA 2022.**

1. Nafurahi kukujulisha kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha Tano katika shule hii mwaka **2022** mchepuo (tahasusi) ya _____________ .Shule ya sekondari Kayuki ipo umbali wa kilometa **10** kusini mwa mji wa **Tukuyu.** Usafiri wa basi kutoka mjini **Tukuyu** unapatikana katika kituo cha mabasi **Tukuyu,** nauli ni sh. **1000/=** (elfu moja tu) Shule hii ni ya wasichana tu.

Muhula wa masomo unaanza tarehe **…… Julai 2022.** Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti Shuleni tarehe **……………….** Mwanafunzi atakayechelewa nafasi yake itachukuliwa na mtu mwingine.

**MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA.**

2.1 – Sare ya shule.

(a). Sketi mbili(**2**) za rangi ya **dark blue** iliyokolea, mshono wa sketi-rinda box mbele na nyuma ziwe

ndefu sana. Kitambaa kimeambatanishwa. Zingatia rangi na aina ya Kitambaa kilichoambatanishwa. Endapo kitakuwa tofauti hazitapokelewa.

(b) Rangi ya hijabu (kijuba) ni nyeupe isiyo na urembo (kwa wanafunzi wa kiislam).

(c) Sare ya michezo kwa shule hii ni traki suti nyeusi (Adidas) T - shirt ya dark blue yenye kola na mistari myeupe kwenye kola na mikononi na raba.

(d) Viatu vya shule vyeusi vya kamba visivyo na kisigino kirefu vya kiwi.

(e) Soksi nyeupe jozi mbili au zaidi (ndefu).

(f) Sweta la rangi ya kijani kibichi lenye mshono wa **V** mbele.

(g). Nguo za kushindia (shamba dress) ni sketi mbili rangi ya **damu ya mzee** ( "kimji") ndefu Sana zenye marinda ya kufukuzana.

(h) Tai rangi ya **dark blue** (ndefu).

2.2. Ada na michango ya shule.

(a) Ada ya shuleni shilingi **70,000/=** (Elfu sabini tu kwa mwaka). Unaweza kulipa sh. **35,000/=** kwa muhula au kulipa zote kwa mkupuo. Fedha hizo zilipwe kwenye Akaunti ya Shule Namba **61401200063** katika Benki ya **NMB** Jina la Akaunti ni Kayuki Secondary School (Tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye pay in slip).

(b) Michango inayotakiwa kulipwa na kila mzazi ni

- (i) Shilingi **15,000/=** kwaajili ya ukarabati wa samani.
- (ii) Shilingi **6,000/=** kwaajili ya kitambulisho na picha.
- (iii) Sh. **20,000/=** kwa ajili ya taaluma.
- (iv) Michango kwa malipo ya walinzi, wapishi na vibarua wengine ni sh. **30,000/=.**
- (v) Sh. **2000/=** nembo ya shule.
- (vi) Fedha ya matibabu sh. **11,600/=** kwa mchanganuo kwamba sh. **5,000/=** ni huduma ya kwanza na sh. **6,600/=** bima ya afya **(CHF).** Mwanafunzi asiye na bima ya afya ndiye atakayetakiwa kuja na fedha ya bima ya afya **sh. 6,600/=** (Aje nayo mkononi)
- (vii) Magodoro ya kukodi yanapatikana shuleni Tsh. **8,000/=** kwa muhula endapo mzazi atahitaji (Siyo lazima).
- (viii) Fedha ya tahadhari sh. **5,000/=** (haitarejeshwa).
- (ix) Fedha ya mtihani wa utamilifu (mock) **20,000/= (**Ilipwe atakapoingia kidato cha sita).

Ada na michango kwa muhula wa kwanza ni sh. **126,000/=.** Ilipwe kwenye **A/C 61401200063 NMB.**

**NB.** Ada na michango yote ilipwe kuanzia tarehe ……………………

(c) Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni ni:-

- (i) Ream **1** ya karatasi ( kwa mwaka).
- (ii) Vitabu vya masomo ya tahasusi husika.
- (iii) Dissecting kit kwa wanafunzi wa Baolojia.
- (iv) Scientific calculator CASIO FX 991 kwa wanafunzi wa tahasusi za sayansi.
- (v) Mashuka pair **2** (pea, pink na pea **1** Light blue), blanketi **1,** foronya **2** pink na light blue, chandarua**1** (rangi yoyote).
- (vi) Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe).
- (vii) Ndoo **2** ndogo zenye mfuniko.
- (viii) Ufagia **1** wa chelewa**,** blashi ngumu yenye mshikio mrefu na blashi ya kusugulia masinki ya choo.
- (ix) Aje na daftari tisa **(9)** quire 3, kalamu na mkebe wa Hisabati.
- (x) Aje na grafu paper mbili **(2)** kwaajili ya mazoezi.

(xi) Aje na Tranka.

## 3. MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULENI.

(i) Wizi.
(ii) Kuto hudhuria masomo kwa zaidi ya siku **90** bila taarifa/utoro.
(iii) Kugoma na kuhamasisha mgomo.
(iv) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.
(v) Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au na mtu Yeyote yule.
(vi) Kusuka nywele kwa mtindo usio kubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wa wapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi ulio kubalika na uongozi wa shule.
(vii) Kufuga ndevu.
(viii) Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.
(ix) Uvutaji wa sigara.
(x) Uasherati, uhusiano wa jinsi moja, kuoa au kuolewa.
(xi) Kupata ujauzito au kutoa mimba.
(xii) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote Yale yanayo vunja sheria za nchi.
(xiii) Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana.
(xiv) Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
(xv) Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
(xvi) Kudharau Bendera ya Taifa.
(xvii) Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.
(xviii) Uharibifu wa mali ya Umma kwa makusudi.

**4. VIAMBATISHO NA FOMU HUSIKA.**

(a) Fomu ya uchunguzi wa Afya (medical Examination form) ambayo itajazwa na mganga Mkuu wa hospitali ya serikali.
(b) Fomu ya Taarifa binafsi ya mwanafunzi.
(c) Fomu ya Taarifa binafsi ya mzazi.

**5. TAFADHALI SOMA KWA MAKINI MAELEZO/MAAGIZO HAYA NA KUYATEKELEZA KIKAMILIFU.** .

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

Saini ya Mkuu wa shule ………………………………..,

Jina la Mkuu wa shule ………………………………….,

Mhuri wa Mkuu wa shule ………………………………,

## TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI

1. JINA KAMILI ………………………………………………………………………..

2. TAHASUSI/MCHEPUO …………………………………………………………...
3. SHULE YA SEKONDARI ALIYOMALIZA KIDATO CHA IV ……………………

Mimi ……………………………………… nimesoma na kuelewa makosa yote
Yatakayo sababisha kufukuzwa shule. Hivyo naahidi kufuata sheria zote za shule, na
Kutojihusisha katika migomo, fujo na makosa yoyote ya jinaii kiwa ni pamoja na kukutwa na
Simu na laini kwa muda wote nitakao kuwa hapa shuleni.

**……………………………………..**
**SAHIHI YA MWANAFUNZI**

………………………………………

### TAARIFA ZA MZAZI

**1. JINA KAMILI LA MZAZI ……………………………………………..**

ANUANI KAMILI …………………… NAMBA YA SIMU ……………………

KIJIJI ……………………. KATA …………………… WILAYA ………………….. MKOA ………………..

**MKATABA WA MZAZI.**

Mimi mzazi wa ………………………. Nakiri kukubaliana na sheria kanuni na taratibu
Za shule hii kiwa ni pamoja naulipaji wa ada na michango kwa wakati kusimamia
Nidhamu ya mtoto na maelekezo mengine yatakayo tolewa na shule kwa kipindi chote
Ambacho mtoto wangu atasoma katikashule hii _____________________
jina ____________________________________ sahihi ______________

**2. MAJINA YA WATU WANAORUHUSIWA KUMTEMBELEA/KUMCHUKUA MTOTO.**

| JINA | UHUSIANO | NAMBA YA SIMU |
|---|---|---|
| …………………………. | ……………………….. | ……………………. |
| …………………………. | ……………………….. | ……………………. |
| …………………………. | ……………………….. | ……………………. |

**3. JINA KAMILI LA AFISA MTENDAJI WA KIJIJI**

JINA ……………………………………….. SAHIHI ……………………….

NAMBA YA SIMU ………………………

## TARATIBU ZA SHULE HII.

1. Mwanafunzi haruhusiwi kuwasiliana na mzazi moja kwa moja kwa masuala Yanayo muhusu Mzazi atajulishwa masuala yote na uongozi wa shule.
2. Mwanafunzi atapata huduma zote za kiroho ndani ya eneo la shule.
3. Hakuna ruhusa ya mwanafunzi kutoka nje ya eneo la shule bila kibali maalum. Kama Nimatibabu atasindikizwa na Matron.
4. Hakuna siku ya wanafunzi kwenda kutembea nje ya shule (Outing day). Mahitaji Muhimu yote yatapatika na shuleni.
5. Mwanafunzi haruhusiwi kutembelea nyumba za watumishi.
6. Mwanafunzi haruhusiwi kuwa na pasi ya umeme na kamera.
7. Mwanafunzi haruhusiwi kusuka nywele.

# OFISI YA RAIS
# TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
# HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE

SHULE YA SEKONDARI KAYUKI,

SIMU Na0745774269 S. L. P. 232,
**TUKUYU.**
Fax.................................
Kumb. Na. KAY/SS/FS/554/VOL3/

Tarehe ………………

ANUANI YA MZAZI/MLEZI
.........................................
......................................
..................................
Tarehe ............................

MKUU WA SHULE,
SHULE YA SEKONDARI KAYUKI,
S.L.P 232,
**TUKUYU**.

**YAH: HATI YA KUKUBALI MASHARTI KUHUSU MTOTO WANGU KUSOMA SEKONDARI YA KAYUKI.**

Mimi .......................................................................................... Mzazi/mlezi wa mwanafunzi ............................................................

Ninakubali mtoto wangu asome shule ya sekondari Kayuki iliokoWilaya ya Rungwe kwa Kufuata masharti yafuatayo,

1. Kwamba mtoto wangu atahudhuria masomo kama kawaida kufanya shughuli nyingine Zote za shule tangu kidato cha **TANO** mpaka kidato cha **SITA**, na atazingatia sheria na Taratibu zote za shule.
2. Nakubali masharti na gharama zilizotolewa katika barua ya kuitwa kwa mwanafunzi (joining instructions) na nitayatimiza kwa wakati unaotakiwa.
3. Nitahakikisha atafika shuleni kwa kufuata tarehe zilizopangwa kwa kipindi chote cha Miaka miwili.

**...........................................** **..................................................**

**TAREHE** **SAINI YA MZAZI/MLEZI**

# THE PRESIDENT'S OFFICE
# REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
# RUNGWE DISTRICT COUNCIL

KAYUKI SECONDARY SCHOOL,
P.O. BOX 232,
**TUKUYU.**

TO.
MEDICAL OFFICER,
……………………………………
…………………………………….
……………………………………..
Please examine
………………………………………………………………………………………
As to her fitness for pursuing further education in this school.

1. Haemoglobin ……………………………………………………………….
2. P.V. Bleeding ……………………………………………………………….
3. Sight …………………………………………………………………………
4. Blood pressure ………………………………………………………………
5. Urine for sugar and pregnancy tests ……………………………………..
6. Stool routine examination …………………………………………………..
7. Asthma ………………………………………………………………………
8. Skin diseases ………………………………………………………………
9. Leprosy ……………………………………………………………………….
10. Epilepsy ……………………………………………………………………
11. Pulmonary tuberculosis ……………………………………………………
12. Deformity …………………………………………………………………..
13. Mental problem …………………………………………………………….
14. Comments …………………………………………………………………

Sign ………………………

Offical stamp.